**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Namba za Simu…………………..**

Mkuu wa Shule. **0624051320**

Makamu Mkuu wa Shule **0769569914/0784622564**

Matron/Patron. **0758141507/0752412341**

Shule ya Sekondari **TUMATI**

S.L.P.**197, MBULU**


Tarehe, 13.06.2023

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI TUMATI HALMASHAURI YA MBULU (DC) MKOA WA MANYARA MWAKA 2023/2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya **CBG/CBA**

Shule ya Sekondari TUMATI ipo umbali wa Kilometa 7 Mashariki mwa Mji wa **DONGOBESH.** Usafiri wa bodaboda/bajaji kutoka mjini DONGOBESH unapatikana katika kituo cha mabasi **DONGOBESH** Nauli ni Shilingi **3000/=** kwa pikipiki na Shilingi **1000/=** kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14.08.2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **14.08.2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **30.08.2023**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **shati nyeupe (2)** mikono mirefu,**sketi (2)** rangi ya blue (dark blue) lenye rinda (boksi) urefu chini ya magoti, **suruali (2)** rangi ya bule (dark blue) na **sweta** rangi ya blue (dark blue) kwa wasichana.
ii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni **nyeupe** ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama itakayotumika darasani na hijabu nyeusi ya kushindia.
iii. Sare ya Michezo ni **T-shirt** ya rangi ya blue, **sketi rangi blue (mshono wa mwavuli), skin tight nyeusi, na raba za michezo jozi moja** Kwa wasichana.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili **nyeupe** za shule.
vi. Nguo za kushindia **track nyeusi moja**, shamba dress-**sketi rangi ya blue bahari(kitambaa kizito mshono wa rinda boksi** na t-shirt rangi kijivu lenye kola.
vii. Ndala za kuogea
viii. Tai rangi ya dark blue
ix. T-shirt- (Zinapatikana karibu na shule)

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

**i.** Madaftari makubwa 10 **(counter- book quire 3)**
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. **Mkebe wa hesabu (mathematical set) kwa tahasusi zote**
iv. Begi la kubebea daftari na vitabu
v. Madaftari madogo ya mazoezi
vi. Kalalmu, penseli za kutosha, rula na kifuto

vii. Aje na Vitabu vya ziada kulingana na tahasusi husika
viii. Dissecting **Kit** na **tray** yenye **nta** kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
ix. Scientific Calculator;(FX 991 MS) Kwa tahasusi zote.
x. Godoro moja size 2 $^{1/2}$ x3x6
xi. Mashuka Jozi 2 **blue 1** na **pink 1**, blanket 1, mto na foronya la blue na pink
xii. Tranka moja na ndoo ndogo 3
xiii. Nguo za ndani za kutosha;
xiv. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xv. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xvi. Vifaa vya usafi hard broom 1, squeezer 1 chelewa (fagio) 1 na jembe 1 na ufagio wa ndani 1.
xvii. Vyombo vya chakula sahani1 bakuli 1 (bati) na kijiko 1.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | **Mchango wa uboreshaji wa taaluma(kwa mwaka)** | **20,000/=** |
| .2 | **Tahadhari(kwa mwaka)** | **5,000/=** |
| .3 | **Nembo(mara moja)** | **2,000/=** |
| 4 | **Kitambulisho cha Shule(mara moja tu)** | **6,000/=** |
| 5 | **Mishahara ya watumishi wa muda(mwaka)** | **20,000/=** |
| **6** | **Mishahara ya wapishi(mwaka)** | **20,000/=** |
| **7** | **Samani(kwa mwaka)** | **15,000/=** |
| **8** | **Mitihani ya utamirifu(kwa mwaka)** | **20,000/=** |
| **9** | **Bima (kwa mwaka )** | **50,400/=** |
| **10** | **Huduma ya kwanza(mwaka)** | **10,000/=** |
| | **Jumla Kuu** | **168,400/=** |

**N.B Fedha zote zilipwe katika benki isipokuwa fedha ya tahadhari, huduma ya kwanza na bima ya afya ziletwe kwa mkono. Aidha mwanafunzi mwenye bima ya afya NHIF Hahusiki na ulipaji wa bima.**

**ACCOUNT NAMBA YA SHULE: 41201200078**

**JINA LA ACCOUNT: TUMATI SEKONDARI**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………

Jina la Mkuu wa Shule, **EUGEN, M.P**

Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA**

**SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule   0624051320**
- **Makamu Mkuu wa Shule, 0769569914/0784622564**
- **Mwandamizi Taaluma, 0784029490**
- **Mwandamizi Malezi   0769621918**

**6.0 FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA / WILAYA AU HOSPITALI NYINGINE ZINAZOTAMBULIWA NA SERIKALI, NA MWANAFUNZI AJE NA HII FOMU PINDI ANAPORIPOTI.**

Mimi / Jina la Mganga ……………………………………………………………………………………..
Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la Mwanafunzi……………………………………………..
Amepima kikamilifu na kuonekana kuwa ana/hana afya nzuri kwa mujibu wa Taarifa zifuatazo"

**A: HALI YA MWILI**

i. Mapigo ya moyo …………………………………………………………………………..
ii. Haemoglobin HB …………………………………………………………………………..
iii. Kundi la damu (Blood Group) …………………………………………………………..
iv. Mkojo (Urine) ……………………………………………………………………………
v. Kinyesi (Stool) …………………………………………………………………………..….
vi. Macho (yana kasoro) Eye test ……………………………………………………………
vii. Masikio (yana kasoro) ……………………………………………………………………….
viii. Ujauzito (Check Cases of Pregnancy) ………………………………………………………

Angalia:- Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i – viii)
………………………………………………………………………….……………………………
…………………………………….…………………………………………………………………
……………..………………………………………………………………………….………………
…………………………………………………………..……………………………………………
…………………………..………………………………………………………………………….

**B. MAGONJWA**

Amewahi / hajawahi / ana / hana magonjwa yafuatayo:-

a) Pumu ( Arthma) …………………………………………………………………………….
b) Kifua kikuu (TB) …………………………………………………………………………….
c) Kifafa (Epilepsy) …………………………………………………………………………….
d) Shinikizo la damu la juu/chini (Blood Pressure) ………………………………………………
e) Vidonda vya tumbo (Ulcers) ………………………………………………………………….
f) Maradhi ya zinaa …………………………………………………………………………….
g) Ukoma (Leprosy) …………………………………………………………………………….
h) Ugonjwa wa akili (mental illness) ……………………………………………………………
i) Maradhi mengineyo makali ambayo hayajatajwa hapo juu kama yapo …………………………

**N.B KATA ISIYOHUSIKA**

**7. A - FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI KUKIRI NA KUTOA AHADI YA UTII YA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi ………………………………………………………………. Wa kidato cha ……………

Nimesoma na kuelewa fomu na maagizo yaliyoambatanishwa juu, utaratibu, kanuni za shule na sheria zake. Endapo nitapatikana na makosa yanayohusiana na vifungu vilivyoorodheshwa kwenye fomu ya kujiunga na shule hii, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu kulingana na vifungu hivyo muda wote niwapo shuleni ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

| | |
|---|---|
| ………………………… | ……. …………………………….. |
| Saini ya Mwanafunzi | Saini ya Mkuu wa Shule |
| Tarehe ……………………… | Tarehe ……………………… |

**7. B FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKUBALI KUSHIRIKIANA NA UONGOZI WA SHULE.**

Mimi ………………………………………………………………………………….

Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………… nimesoma na kuelewa maagizo yaliyotolewa na uongozi wa shule. Ninakubali na ninaahidi kutekeleza maagizo yaliyotolewa, vile vile nitatoa ushirikiano kwa uongozi wa shule kwa malezi ya watoto wangu.

……………………….

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

Tarehe ……………………

**N.B** Unatakiwa kuzingatia mambo ya muhimu ya msingi katika sheria za shule na utafafanuliwa kwa undani mara baada ya kuripoti shuleni.

**MAMBO YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI MARA ANAPORIPOTI SHULENI.**

1. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali/ Hospitali nyingine zinazotambuliwa na Serikali.
2. Fomu ya mwanafunzi kukiri na kutoa ahadi ya utii muda wote atakapokuwa shuleni.
3. Fomu ya Mzazi/Mlezi kukubali kushirikiana na Uongozi wa shule katika malezi ya mtoto wake.
4. **UNAPORIPOTI UNATAKIWA KUJA NA BARUA YA MAAGIZO (JOINING INSTRUCTIONS) ILIYOJAZWA KIKAMILIFU, VYETI VYAKO VYA TAALUMA (RESULT SLIP NA CHETI CHA KUZALIWA)**